

# **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



## **MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

### **DIVISHENI YA KAZI**

### **DAR ES SALAAM**

## **TAARIFA MUHIMU**

### **YAH: UENDESHAJI WA MASHAURI YA MIGOGORO YA KIKAZI MAHAKAMA KUU KITENGO CHA KAZI DAR ES SALAAM KUANZIA JUMATATU TAREHE 30/03/2020**

Kufuatia mlipuko wa Virusi vya Korona (COVID-19) na hatua za tahadhali zilizotangazwa na Serikali pamoja na Mahakama ya Tanzania, Mahakama hii itaendesha mashauri yake kwa utaratibu ufuatao; kama sehemu ya hatua za kupunguza mkusanyiko wa watu wengi mahakamani:-


1. Katika mashauri yote ya kutajwa, wahasika (wadaawa, mawakili na wawakilishi binafsi) hawatatakiwa kuhudhuria mahakamani katika kipindi chote cha tahadhali kilichotangazwa na Serikali au

mpaka itakapoelekezwa vinginevyo. Wahusika watapata Taarifa za tarehe za mashauri yao kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi (sms notification) na/au kupitia mfumo wa JSDS2.

2. Kwa mashauri yaliyopangwa kwa kusikilizwa ambayo yana wadaawa wengi, wadaawa watawakilishwa na mtu mmoja mmoja tu na yale yenye mawakili au wawakilishi binafsi, mawakili au wawakilishi binafsi ndio wataruhusiwa kuingia mahakamani; na wahusika watatakiwa kufika mahakamani kwa **wakati/muda** uliopangwa kuanza usikilizwaji wa mashauri yao.
3. Kwa mashauri ya utekelezaji (execution) yenye maombi ya marejeo, wahusika wasifike mahakamani. Taarifa ya tarehe za mashauri yao zitatolewa kwa ujumbe mfupi (sms) na/au kupitia mfumo wa JSDS2.
4. Mashauri yote yaliyopo katika masjala ndogo ya Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi Morogoro, wahusika hawatatakiwa kufika mahakamani na taarifa ya tarehe za mashauri yao watazipata kwa ujumbe mfupi na/au mfumo wa JSDS2.

5. Mwakili wanahimizwa na kusisitizwa kuendelea **kujisajili** na **kutumia** njia ya kieletroniki katika kuwasilisha mashauri mahakamani.
6. Wahusika wa mashauri mbalimbali mahakamani wanatakiwa kuhuisha (update) namba zao za simu zilizopo kwenye kumbukumbu za kimahakama kama zina mabadiliko au hazipatikani.

\* Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa ujumbe mfupi (sms), simu Na. **0744 000 760** na/au barua pepe **Laborcourt@judiciary.go.tz**



**S.R. DING'OH**  
**NAIBU MSAJILI MFAWIDHI**  
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**  
**DIVISHENI YA KAZI**

26/3/2020